

# JIMBO KUU KATOLIKI LA DAR ES SALAAM



**PAROKIA YA KUNG'ARA KWA YESU KRISTO, MBEZI MSHIKAMANO**

S.L.P. 280 D'SALAAM, +255 686 794177, E: katolikimshikamano@gmail.com

## MATANGAZO: DOMINIKA YA 3 YA PASAKA - TAR. 19.04.2026

| | | |
|---|---|---|
| 1. | **LEO DOMINIKA 19.04.2026** | **DOMINIKA YA 3 YA PASAKA MWAKA A**<br>**Mchango wa Pili ni kwa ajili ya BIBLIA** |
| 2. | **JUMAMOSI 25.04.2026** | Jumamosi ijayo ni siku ya kusali katika Kanda. Kanda zinaombwa kuhakikisha zinakamilisha mapengo yote ya uongozi katika VMJ.<br>***Angalia Ratiba ya sehemu ya kusali katika Kanda.*** |
| 3. | **DOMINIKA 26.04.2026** | **DOMINIKA YA 4 YA PASAKA MWAKA A**<br>**Misa ya 1: Saa 12:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Mt. Martha<br>Watangaza Neno: Pius Laswai na Theresia Emmanuel<br>**Misa ya 2: Saa 2:30 asubuhi**<br>Wasimamizi: Mt.Katarina wa Siena<br>Watangaza Neno: Baptis Komba na Emmanuel Raphael<br>**Misa ya 3: Saa 11:00 Asubuhi**<br>Wasimamizi: Mt. Martha na Mt. Katarina wa Siena<br>**Mchango wa pili kwa ajili ya Ujenzi** |
| 4. | **SUNDAY SCHOOL** | Jumuiya itakayokuwa Zamu kuhudumu kwenye Sunday School Dominika ijayo 26.04.2026 kwenye Chai na baadaye kuungana na Jumuiya zilizopo zamu kusimamia kwenye Misa ya watoto ni Mt. Gregory VII. Mt. Yohane Krisostom wajiandae kwa Dominika inayofuata 03.05.2026. |
| 5. | **UCHAGUZI WA VMJ NGAZI YA JNNK** | Jumuiya zote ambazo hazina viongozi wa VMJ vya UWAKA, WAWATA, VIWAWA & WAZEE NA WASTAAFU zichague walau viongozi watatu (3) na kuleta taarifa Parokiani. Zitumie mkutano ujao wa Kanda kukamilisha |
| 6. | **HARAMBEE MAALUM** | Harambee maalum kukamilisha ukumbi wa Parokia na rangi jengo la Kanisa iliyofanyika 22.02.2026. Waamini ambao hawakushiriki wanaweza kutoa ahadi zao kwa viongozi wa Jumuiya au viongozi wa Kamati Tendaji Parokia. Kila Jumuiya inaombwa kuchukua fomu ya kuwasilisha taarifa kamili ya kila wiki. Wote walioahidi wanakumbushwa kukamilisha ahadi zao na mwisho ni 30.04.2026. |
| 7. | **MCHANGO WA KILA WABATIZWA Tshs. 2,000** | Waamini wanakukushwa mchango wa kila Mbatizwa wa Tshs. 2,000 au zaidi kwa ajili ya ujenzi wa Kanisa Mbadala - Pugu awamu ya tatu 2026. Viongozi wa kila Jumuiya wachukue fomu maalumu iliyotolewa na |

| | | |
|---|---|---|
| | | Jimbo ofisini kwa Karani. Mwisho wa kuwasilisha ni tarehe 31.05.2026 |
| 8. | **CHAKULA CHA HISANI KUCHANGIA UJENZI WA KANISA KUU MBADALA** | Baba Askofu Mkuu Mhashamu Sana wa Jimbo Kuu a DSM Thaddeus Ruwa'ichi anawashukuru wote walijitokeza katika chakula cha hisani kuchangia ujenzi wa Kanisa Kuu Mbadala 17.01.2026 na kwa namna ya pekee anapenda kuwakumbusha wote waliotoa ahadi kukamilisha ahadi zao na kutuma jimboni bank slip za michango yao.<br>Aidha tumetambua kwamba wachangiaji binafsi wenye nia ya kufanya hivyo bado ni wengi sana. Hivyo, ili kuratibu vizuri uchangiaji wa watu binafsi na kushirikisha wachangiaji wengi zaidi tumekubaliana tuwe na Fundraising zaidi ya moja na zifanyike katika Dekania yetu ya MT. Augustino Mbezi Louis itafanyika tarehe 20.06.2026. Waamini wote wenye uwezo wa kuchangia Tshs. 500,000 na zaidi wanalikwa kujitokeza kushiriki kazi hii ya ujenzi huo wa Kanisa Kuu Mbadala la Jimbo letu. Utaratibu zaidi utatolewa. |
| 9. | **WARSHA YA WAAMINI WOTE JIMBO KATOLIKI LA DSM** | Idara ya kichungaji Jimbo Kuu la DSM inawaalika waamini wote kushiriki Warsha maalum itakayofanyika tarehe 06.06.2026 katika Uwanja wa Uhuru kuanzia saa 2:00 asubuhi. Ada ya ushiriki kwa kila mshiriki ni **Tshs. 5,000.**<br>**MATUKIO**: Misa Takatifu, Semina na Michezo<br>**MADA:**<br>1. Roho Mtakatifu na Maisha ya Mkristo<br>2. Mkristo na Mazingira (Laudato Si)<br>**KAULIMBIU "Jubilei ya Miaka 75 ya Jimbo Kuu la DSM; Tufanywe Upya na Roho Mtakatifu"** |
| 10. | **UWAKA DAY JIMBO 01.05.2026** | Uwaka Day Jimbo siku ya Mei Mosi itafanyika katika kituo cha Hija Pugu. Ni siku ya wanaume huku wakiadhimisha Sherehe ya Mt. Yosefu Mfanyakazi, Msimammiazi wa Jimbo letu na Utume wa Wanaume. Misa Takatifu itaanza saa 3:00 asubuhi. Wote wanakaribishwa |
| 11. | **KARISMATIKI KATOLIKI** | Karismatiki Katoliki Dekania wameandaa Kambi ya shukurani kuanzia 01/05 -10/05/2025 hapa Parokiani kwetu. Wote wanakaribishwa |
| 12. | **PUGU MARATHONI "UPENDO NA MSHIKAMANO"** | Pugu Marathon itafanyika tarehe 30.05.2026 kuanzia saa 11:00 alfajiri na mbio zitaanzia katika kituo cha Hija Pugu. Mbio hizi ni kwa ajili ya kuchangisha pesa za Ujenzi wa Kanisa Kuu Mbadala. Mwisho wa usajili ni tarehe 20.05.2026 Ada ya ushiriki nin Tshs. 30,000. Unaweza kujisajili kwa njia ya mtandao. Wote tunakaribishwa kuchangia na kushiriki. Kwa maelezo zaidi angalia Tangazo kwenye Ubao wetu (Urefu 2kms, 5km, 10kms na 21kms) **www.pugumarathon.or.tz** |
| 13. | **BAHASHA ZA PASAKA** | Wote waliochukua bahasha za Pasaka wanaomba waanze kuzirudisha na kwa wale ambao bado hawajachukua bahasha bado zipo. Waohudumu zamu watakuwa wanagawa mlangoni. |
| 14. | **GAZETI LA TUMAINI LETU** | Viongozi wa Jumuiya wanakumbushwa kuchukua Gazeti la Tumaini letu ofisini na kufanya malipo ya nakala 4 kati ya 5. |

## TANGAZO LA NDOA KWA MARA YA PILI

1. Emmanuel JOHN LYANGA LAWRENCE Bin LYANGA LAWRENCE KIULA na ELLEN LUSHIBA MGEMA kutoka Parokia ya Majengo - Mhongolo Anatarajia kufunga ndoa na:
   CECILIA PEACE GEORGE BINTI GEORGE KAPONGO LUCIAN na PORTINA ENOCK KIBWANA kutoka Parokia ya Matengo - Mhongolo Kahama wanatarajia kufunga ndoa 02.05.2026 huko Mhongolo Kahama. Wazazi wa Bibi Harusi wanasali hapa Parokiani Mbezi Mshikamano.

**SEMINA YA NDOA:**

1. Msimbazi Center itafanyika tarehe 18/04 na leo 19/04/2026

## MASOMO YA DOMINIKA

## DOMINIKA YA 4 YA PASAKA, MWAKA A - TAREHE 26.02.2026

| | |
|---|---|
| SOMO I | Mdo. 2: 14a, 36 - 41 |
| WIMBO WAKATIKATI | Zab 23: 1-6 |
| SOMO II | 1Pet. 2: 20b -25 |
| SHANGILIO | Yn. 10: 14 |
| INJILI | Yn. 10: 1 - 10 |